



**JAMHURI YA MUUNGANO WA  
TANZANIA OFISI YA WAZIRI  
MKUU-TAMISEMI  
HALMASHAURI YA WILAYA YA MKINGA  
SHULE YA SEKONDARI MARAMBA**



**S.L.P.76Maramba.Baruapepe:marambasecondary20@gmail.com Simu/Contacts:  
Mkuu wa Shule 0713337896; Makamu Mkuu wa Shule 0755426384 na Patron  
0758738711**

**Kumb.Na.MSS/J.2/VOL.I/38.**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi .....**

**S.L.P .....**

**Yah: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA  
SHULE YA SEKONDARI MARAMBA - HALMASHAURI YA MKINGA MKOA  
TANGA MWAKA.....**

**1.Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka.....na atasoma tahasusi ya.....**

Shule ya Sekondari MARAMBA ipo umbali wa Kilometa 54 Magharibi mwa Mji wa TANGA Usafiri wa basi kutoka mjini TANGA unapatikana katika kituo cha mabasi MWEMBE MAWAZO.Nauli ni Shilingi 4000 hadi Maramba Mjini na s h 1500 kwa pikipiki hadi Maramba shuleni.

Muhula wa Masomo unianza tarehe ..... hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe ..... Mwisho wa kuripoti ni tarehe .....

## **2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

### **2.1 Sare za Shule**

- i. Sare ya shule hii ni suruali mbili za heshima rangi ya khaki (polisi)
- ii. Mashati mawili meupe ya mikono mirefu
- iii. Nguo za michezo ni T-shirt za Bluu,kaptula/bukta rangi ya bluu na Raba rangi yoyote.
- iv. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;
- v. Soksi jozi mbili nyeusi za shule;
- vi. Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali;
- vii. Sweta rangi ya maron(damu ya mzee) shingo ya V
- viii. Nguo za kushindia (shamba dress) suruali damu ya mzee (maron) na fulana yenye shingo ya V damu ya mzee (maron).
- ix. Tai ya khaki (polisi)
- x. Tisheti (T-shirt) damu ya mzee (njoo na Tshs 15,000 unaweza kuzipata shuleni ukipenda

### **2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

- i. Madaftari 10 (counter books ni mazuri zaidi).
- ii. Ream (A4) ya Karatasi, Mbili (2) kwa mwaka;
- iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (orodha imeambatishwa)
- iv. Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma Biology;
- v. CBG aje na Scientific Calculator;
- vi. Godoro la sponge lenye foronya futi 2 na nusu kwa 6.
- vii. Mashuka rangi ya blue bahari jozi moja na ya pink jozi moja, Mchandarua kimoja.
- viii. Nguo za ndani za kutosha;
- ix. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
- x. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;
- xi. Kwanja 1, jembe 1, reki 1, mifagio wa ndani,
- xii. CBG aje na Kikamulio/kikaushio Cha maji (Squeezer) moja na brush 1 ngumu(hard broom) ya kusugulia sakafu/tiles
- xiii. HKL aje na brashi Moja ya kusugulia vyoo na brush Moja (hardbroom) ya kusafishia sakafu/tiles.
- xiv. Mwanafunzi aje na Bima ya afya,kama hana Bima ya Afya tafadhali aje na Tshs. 50,400/= .Kwa ajili ya kumkatia Bima ya afya kwa mwaka mmoja;

**NB:** Mwanafunzi haruhusiwi kuja na nguo yoyote ya nyumbani tofauti na sare zilizoainishwa.

**2.3 Michango  
mbalimbali a)  
Shule za Bweni**

<b>Na</b>	<b>Aina ya Mchango</b>	<b>Kiasi</b>
1.	Mchango wa Uendeshaji wa Shule	65,000/=
3.	Tahadhari	5,000/=
4.	Nembo	5,000/=
5.	Kitambulisho cha Shule	5,000/=
	<b>Jumla</b>	<b>80,000/=</b>

**Michango yote ilipwe kwenye account ya shule No 41701200088 (NMB).  
Jina  
la akaunti ni MARAMBA SECONDARY SCHOOL. Lipia Benki ama  
kwa mawakala.**

### **3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

#### **3.1 Sheria na Kanuni za Shule**

- i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
- ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
- iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
- iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
- v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
- vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
- vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
- viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
- ix. Kutunza mali za shule;
- x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
- xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

#### **MUHIMU:**

- ❖ **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**
- ❖ **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**
- ❖ **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa).**

### **3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

- i. Wizi;
- ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
- iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
- iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
- v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
- vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
- vii. Kufuga ndevu;
- viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevyo;
- ix. Uvutaji wa sigara;
- x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuo au kuolewa;
- xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
- xii. Kusababisha mimba;
- xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
- xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
- xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
- xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
- xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
- xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

### **4. Viambatisho na Fomu Muhimu**

- i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
- ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
- iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
- iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**5. Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.**

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

Saini ya Mkuu wa Shule.....  
Jina la Mkuu wa Shule  
**TIMILAI H SHESHANGALI**  
Mhuri wa Mkuu wa Shule.....

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule 0713337896.**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0755426384**
- **Mwandamizi Taaluma 0714781813/0788440161**
- **Mwandamizi Malezi 0758738711**

# SHULE YA SEKONDARI MARAMBA

## KIAPO CHA MZAZI/MLEZI

Nakiri kusoma na kuelewa sheria zote na taratibu zote zilizotolewa na shule hii, naahidi kumsaidia mwanangu katika kumlea na kumhimiza kutii na kufuata sheria na taratibu zote za shule.

1. JINALAMZAZI/MLEZI.....MAHALIANAPOISHI.....  
NAMBA YA SIMU.....SAINI

PICHA

MAJINA YA NDUGU WA KARIBU WA MWANAFUNZI

(1) JINA.....MAHALI ANAPOISHI.....  
NAMBA YA SIMU.....

PICHA


(2) JINA.....MAHALI ANAPOISHI.....  
NAMBA YA SIMU.....

PICHA

(3) JINA.....MAHALIANAPOISHI.....  
NAMBA YA SIMU.....

PICHA

## HISTORIA YA MWANAFUNZI



Jina kamili aliloandikishwa shule	Shule ya msingi na sekondari alizopitia	Tarehe ya kuzaliwa	Mahali alipozaliwa	Dini/Dhehebu	Uraia
	Msingi.....          Sekondari..... .....				

Nakiri kusoma na kuelewa sheria zote na kanuni zote za shule, nakiri kufuata na kutii sheria hizo, naahidi kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.

JINA LA MWANAFUNZI.....SAINI.....

**MUHIMU**

FOMU HII ISAINIWE NA MZAZI NA MWANAFUNZI NA IRUDISHWE SIKU YA KURIPOTI SHULENI.

**GOVERNMENT OF TANZANIA**  
**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

MARAMBA SECONDARY SCHOOL,  
P.O BOX 76  
MARAMBA.

TO; Medical Officer;  
.....

Mr. /Miss..... (Name in full)

Please examine the above named as to his physical and mental fitness for full time schooling course. The examination should include the following categories (I-III) each category sub-category will render the applicant in eligible for the course.

- I.a)Eye sight
- b) Hearing
- c) Limbs
- d) Speech
- e) Venereal diseases
- f) Leprosy
- g) Epilepsy
- II. Neuroses
- III. Other serious diseases

**MEDICAL CERTIFICATE**

(To be completed by Government officer) I have examined the above named and consider that he is physically fit/unfit and mentally fit/unfit for a full time schooling course

- a) Eye sight ..... b) hearing .....
- c) Limbs ..... d) speech.....
- e) Venereal diseases ..... f) Leprosy.....
- ii) Neuroses.....
- iii) Other serious diseases .....

Station ..... Signature .....

Designation ..... Date .....

## MARAMBA SECONDARY SCHOOL

(Recommended books for students to purchase for individual further reading)

S/N	SUBJECT	BOOKS
1	BASIC APPLIED MATHEMATICS	<p>Basic Applied Mathematics by TIE</p> <p>Basic Applied Mathematics By GDY Publisher</p> <p>Pure Mathematics by JK backhouse</p>
2	INORGANIC CHEMISTRY	<p>1.Inorganic part 1&amp;2 by TIE</p> <p>2.Physical chemistry –Mzumbe project</p> <p>3.Chemistry by Chande</p>
3	PHYSICAL CHEMISTRY	<p>1.Physical chemistry by Ramsden</p> <p>2.A- level calculations-Ramsden</p> <p>3.Chemistry by Petrus</p>
4	ORGANIC CHEMISTRY	<p>1.Organic chemistry part (A&amp;B) Mzumbe BK project</p> <p>2.Organic chemistry by Solomoni</p>
5	GEOGRAPHY	<p>1.Pritchard M, John(1971) Practical geography for Africa</p> <p>2.PT Msabila (2007) A comprehensive Approach to Physical Geography for secondary schools</p> <p>3.Msabila DT (2000) An intergrated Focal Regional Study on Human and Economic Geography</p>
6	BIOLOGY	<p>1.Sopper et al – Biological science 3 edition</p> <p>2.Susan Toole &amp;G Toole. Understanding Biology for A- level students</p> <p>3.B.M.V Robert.Biology: A functional approach</p> <p>4. Silvia Mader.Inquiry into life</p>
7	KISWAHILI A. USHAIRI	<p>Nunua vitabu vitatu kutoka kila sehemu (A,B NA C)</p> <p>1.Haji, G,H (1994) Kimbuga Dar es salaam.TUKI</p> <p>2.Khatibu,M (1998) .Fungate ya uhuru,Dar es salaam.Dar es salaam university press.</p> <p>3.Mvungi,(1985) , chungu tamu;Dar es salaam Tanzania Publishing House.</p>

	<p>B. TAMTHILIYA</p> <p>C.RIWAYA</p>	<p>4.H.J Mwansoko Kitangulizi cha Tafsiri nadharia na Isimu</p> <p>5. Rboert S (1970) Mapenzi bora,Dsm; Evance&amp; Brothers LTD</p> <p>1.Hussein,E.(1988) . Kwenye ukingo wa thim; Nairobi Oxford University Press</p> <p>2.Mbogo E (1993) Morani ;Dar es salaam.Dar es salaam Tanzania Publishing House</p> <p>3.Mohamed,S.A (1988) Kivuli kinaishi ; Nairobi Oxford University press</p> <p>4.Penina Mhando ; Nguzo mama</p> <p>1.Msokile, M (1990) Usiku utakapokwisha;Dar es salaam: Dar es salaam University Press</p> <p>2.Robert S (1967) .Kufikirika; Nairobi Oxford University Press</p> <p>3.Shafi,A.S (1997) Vutani kuvute; Dar es salaam. Oxford University press</p> <p>4.Tuwa (2007) Mfadhili;Dar es salaam.Macmillian</p>
8	<p>LITERATURE</p> <p>A.NOVELS</p> <p>B. PLAYS</p>	<p>Please select three books from A &amp; B; Two from C (Poem)</p> <p>1.Arm A.K (1969) The Beautiful One Are Not Born; New York: Collier Macmillan</p> <p>2. Chinua, A. (1988) A Man Of the People, Oxford: Heinemann Education Publishers</p> <p>3. Chinua, A et al (2000) Encounters from Africa. Nairobi. Macmillan Publishers ltd</p> <p>4. Safo, D (1983) . His Excelence The Head oh State. DAR es salaam. Macmillan</p> <p>5. Ndunguru S.N (1999) Divine Providence.Dar es salaam; Mkuki na Nyota Publishers</p> <p>1. Ibsen, H (1967) An Enemy of The People Nirobi. Heinemen Education Books ltd</p> <p>2.Imbuga,F (1976) , Betrayal in the city</p> <p>3.Ngungi wa Thiong’o &amp; Ngungi wa Mirii (1982) I wii Marry When I want Nairobi</p> <p>4. Omtatah ,O (2006) . Lwanda Magere . Dar es Salaam. Mkuki na Nyota Publisher</p> <p>5. M bukenya, A (2004) .Rugan.J (2005) . Black Mamba .Dar es salaam</p>

	C. POEMS	<p>Mkuki na Nyota Publishers</p> <p>6. The bridge. Dar es salaam Mkuki na Nyota Publishers</p> <p>1. Mloka , C (2005) The Wonderful Surgeon and other Poems. Dar es salaam: Mkuki na Nyota Publishers</p> <p>2. Tanzania insititute of Education (1996) Selected Poems. Dar es salaam Tanzania Insititute of Education</p>
9	ENGLISHI ONE	1.High Schools Grammer and composition By Aren & Martin
10	G/STUDIES	<p>1.General Studies For Secondary School By Mbalase , R</p> <p>2.General Studies By SETA</p>
11	HISTORY	<p>1.How Europe underdeveloped Africa By Walter Rodney</p> <p>2.General History of Africa By AssaOkot</p> <p>3. Contemporary Historical Event- Vol. I &amp; II By Shibital C. K Tumain</p> <p>4. The Revolutionary Year , West Africa since 1800- B y Webster J B &amp; Boachen A. A</p> <p>5.Mastering Modern World History –By Norman lowe</p>